EFATHA MINISTRY

P.O. Box 9332, Tel: 255-22-2773535; Fax: +255-22-2772579
Dar es Salaam, Tanzania, East Africa.
E-mail: efatha@muchs.ac.tz, efatha2001@yahoo.com

OUR REF: EM/A.42/GC/VOL.2/133
DATE: 11th April , 2012

1. UVAMIZI WA POLISI NDANI YA KANISA LA EFATHA MWENGE

Tarehe 9 Aprili 2012, jumatatu ya pasaka, majira ya saa kumi na mbili asubuhi waumini wa Efatha walikuwa katika ibada ya morning glory katika kanisa la Efatha Mwenge wakiongozwa katika ibada hiyo na Mchungaji David Mwakisole ndani ya kanisa. Kanisa limezungushiwa ukuta pande zote nne na lina mageti ya kuingilia kanisani ambayo yanafungwa. Polisi walipanda ukuta wakachungulia wakasikika wakisema hawa huku ndani. Baadae polisi wakarukia ndani kupitia ukutani. Wakati ibada inaendelea ghafla waumini walivamiwa kutoka nje na watu ambao baadae walitambuliwa kuwa ni polisi. Walipoingia kwa nguvu wakatupa mabomu ya machozi ndani ya kanisa huku wakifyatua risasi za moto wakati ibada ikiendelea. Kwa kitendo hicho ibada ilivurugika na kusimama na waumini wakaanza kukimbia ovyo ndani ya kanisa. Risasi na mabomu ya machozi yalitupwa kuelekea madhabahuni na kuelekea kwa waumini waliokuwa katika ibada.

Waumini wengine waliokuwa wakija kwenye ibada walizuiliwa nje na kukamatwa. Kilichofuata ni vurugu huku waumini wakikimbia na polisi wakiwapiga kwa virungu, vitako vya bunduki na mateke. Baadhi ya waumini walijeruhiwa vibaya sehemu mbalimbali za mwili na ukumbi wa kanisa ulitapakaa damu. Pia polisi walivunja madirisha, viti, milango na spika kama ilivyoonyeshwa katika baadhi ya vyombo vya habari hasa ITV. Kabla hawajavamia, mmoja wa askari aliwatahadharisha wenzake kuwa wasipige mabomu na risasi kwa kuwa hapo ni kanisani lakini wenzake walipinga wakisema kuwa huyu mtu ana kiburi na watu hawa ni wakorofi. Wakati risasi na mabomu yakipigwa baadhi ya askari walikuwa wakiokota maganda ya risasi na mabaki ya mabomu ya machozi ili kuondoa ushahidi. Hata hivyo baadhi ya risasi za moto, maganda ya risasi za moto na mabaki ya mabomu yalibaki kanisani na yamehifadhiwa mahali maalum kwa hatua zaidi.

Kanisani kulikuwa na idadi ya waumini kati ya sitini na sabini waliokuwa wanaabudu. Polisi waliwakamata jumla ya waumini 53 pamoja na wachungaji waliokuwa wakiongoza ibada wakiwapiga na kuwasweka katika magari ya polisi kuwapeleka kituoni pamoja na kuvuta gari zilizokuwa zimeegeshwa nje ya kanisa kwa breakdown. Tumepata habari kuwa walikuja na baadhi ya waandishi wa habari walioandaliwa kabla ili kurekodi tukio hilo na ushahidi tunao. Kwetu sisi inaonyesha kuwa tukio hilo liliandaliwa kwa makusudi ili likatekelezwe katika kanisa la Efatha. Tukio hili linatupa hisia kuwa kuna chuki kubwa kwa Huduma ya Efatha.

Kitendo cha polisi kuvamia na kuvuruga ibada ni kinyume na sheria na katiba ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyoweka uhuru wa kuabudu na sheria za nchi zinazoeleza kwamba ibada zisiingiliwe. Tunajiuliza kulikuwa na tatizo gani polisi wasisubiri nje ibada iishe na wawachukue watu wanaotaka kuwachukua. Ndani ya kanisa hakukuwa na vita, wala mtu mwenye silaha, wala mtu anayeuawa ambaye polisi walilazimika kwenda kumwokoa. Sisi tunaliona hili kuwa ni kumdharau Mungu, kuvuruga ibada na kuwadhalilisha waumini wa Efatha waliokuwa wakitumia uhuru wao wa kuabudu. Leo wamefanya hivyo kwa dharau ndani ya kanisa la Efatha, kesho tutegemee watakwenda kufanya nini kwa dhehebu jingine, Msikiti, Dini nyingine au watu waliokusanyika kihalali na kwa sababu halali?

2. MUJUMUISHO:

Kwa kitendo hiki cha kudhalilisha Imani, tunaenda wapi?

EFATHA FOUNDATION LTD
P.O BOX 32174, MWENGE, DAR ES SALAAM
TELEPHONE: +255732993196, FAX:+255732993196
WEBSITE: www.efathafoundation.org
EMAIL: efathafoundationltd@yahoo.com / info@efathafoundation.org
OUR REF: EFL/ADMN/4/2012
TAREHE 11/4/2012

TAARIFA KWA UMMA

1. UMILIKI WA KIWANJA NA. 90, ENEO LA MWENGE (NURU CENTRE)

1.1 Utangulizi

Tarehe 9 mwezi April 2012, Jumatatu ya Pasaka,baadhi ya vyombo vya habari vilitangaza habari ya umiliki na matukio yaliyotokea katika eneo hilo. Habari zilizotangazwa ni za upande mmoja na hazina usahihi. Huduma ya Efatha inapenda kuelezea umma taarifa sahihi juu ya upatikanaji wa kiwanja na 90, umiliki na matukio yaliyotokea katika eneo hilo.

1.2 Upatikanaji na umiliki wa eneo

Serikali kupitia Tume ya Kurekebisha na Kubinafsisha Mashirika ya Umma (PSRC) ilitangaza zabuni ya uuzwaji wa eneo la Mang'ula Mechanical and Machine Tools Company Ltd iliyofilisika, Kiwanja namba 90, Mwenge katika magazeti ya Uhuru na Daily News ya tarehe 4 mwezi Mei 2005.

Tarehe 18 Mei 2005, huduma ya Efatha kupitia kitengo chake cha uchumi, Efatha Foundation Ltd, kilipeleka maombi ya zabuni ya kununua eneo hilo PSRC.

Efatha Foundation Ltd ilipokea barua kutoka PSRC yenye kumbukumbu Na. PSRC/1/13/93 ya tarehe 30 Mei 2005 ikiarifu kwamba zabuni yetu ya kununua eneo hilo imeshinda kwa kiasi cha shilingi za kitanzania milioni mia nne.

Masharti ya Malipo ya zabuni yalikuwa asilimia kumi ilipwe wakati wa kupeleka maombi na asilimia tisini ilipwe ndani ya miezi mitatu baada ya kushinda zabuni.

Efatha Foundation Ltd ililipa shilingi milioni arobaini yaani asilimia kumi ya bei siku ya kupeleka maombi ya zabuni kwa hundi Na. 000261 ya benki ya Azania na kupewa risiti ya PSRC Na. 6956 ya tarehe 31 Mei 2005. Na shilingi milioni mia tatu sitini ililipwa kupitia hundi Na. 000319 ya benki ya Azania ambayo ni asilimia tisini tarehe 10 mwezi Juni 2005 na kupewa risiti ya PSRC Namba 6984 na hivyo malipo yote yakawa yamekamilishwa.

Baada ya kukamilisha malipo Efatha Foundation Ltd ilikabidhiwa hati miliki Namba 41641 ambayo ilipelekwa wizara ya Ardhi ili ibadilishwe jina kutoka mmiliki wa mwanzo na kuandikishwa jina la Efatha Foundation Ltd. Kwa hiyo Serikali ikahamisha umiliki kutoka Mang'ula Mechanical and Machine Tools Company Ltd iliyofilisika kwenda Efatha Foundation ltd tarehe 15 Novemba 2005 saa sita kamili mchana kwa uhamisho Namba 98648.

Kabla ya Huduma ya Efatha kununua eneo hilo kulikuwa na wavamizi ambao ni makampuni na watu binafsi kumi na moja ambao walikuwa wamewekwa katika eneo hilo na Mang'ula Mechanical and Machine Tools Company Ltd iliyofilisika bila kibali cha mfilisi yaani PSRC. Kwa kuwa hawakuwa wapangaji halali walikuwa wavamizi (trespassers). Wavamizi hao wakapewa notisi ya kuondoka na PSRC lakini hawakuondoka. Baadae shughuli za mfilisi, PSRC, zikachukuliwa kisheria na Consolidated Holding Corporation (CHC). CHC nao wakawapa wale wavamizi notisi kuwa waondoke kwa sababu eneo hilo limeuzwa lakini hawakuondoka. Efatha Foundation Ltd ilipomiliki eneo hili kihalali na kisheria wakawapa wavamizi notisi ya kuondoka mwaka 2005, wavamizi nane wakatii amri wakaondoka na wavamizi watatu walikaidi kuondoka ambao ni pamoja na Afro Plus Industries Ltd.

Baada ya hapo wavamizi watatu waliokataa kuhama wakafungua kesi mahakamani dhidi ya Efatha Foundation Ltd wakipinga kuhamishwa.

Ni vyema ieleweke kuwa Efatha Foundation Ltd iliponunua eneo hili thamani yake ilijumuisha majengo yaliyokuwa yamejengwa humo na Mang'ula Mechanical and Machine Tools Company Ltd iliyofilisika. Hii ni pamoja na jengo alilokuwa anatumia Afro Plus Industries Ltd ambalo linalalamikiwa kubomolewa na kwamba tumeharibu mali. Jengo lililobomolewa ni mali ya Efatha Foundation Ltd na siyo mali ya Afro Plus Industries Ltd kama ilivyodaiwa.

1. **MAJUMUISHO**

Vielelezo vyote kuhusu umiliki wetu halali wa eneo hili vilishawasilishwa polisi mkoani na wilayani. Kutokana na maelezo haya Efatha Foundation Ltd inapenda kuuthibitishia umma kuwa EFATHA FOUNDATION LTD ndiyo mmiliki halali wa KIWANJA NA. 90, ENEO LA MWENGE (NURU CENTRE) na si vinginevyo.

.....

KATIBU

EFATHA FOUNDATION LTD